NGAO YA FASIHI

(SEHEMU YA A-MASWALI YA VITABU TEULE NA FASIHI SIMULIZI)

(MAJIBU KSH. 200 KWA 0707311302-KURASA 92)

CHOZI LA HERI

KIGOGO

TUMBO LISILOSHIBA

FASIHI SIMULIZI

NA

MWALIMU ONYANGO

TOLEO LA 1, 2020

TABARUKU KWA WATAHINIWA WOTE WA KCSE, MWAKA WA 2021

© 2020 MWALIMU ONYANGO 0707311302

KUHUSU NGAO YA FASIHI

Ngao ya Fasihi ni kitabu cha kipekee kuwahi kuandikwa katika kipindi hiki cha likizo. Kitabu hiki kina maswali takribani mia 500 kutoka katika vitabu teule pamoja na fasihi simulizi na majibu yake. Lengo la kitabu hiki ni kumwelewesha mwanafunzi wa fasihi zaidi hasa mtahiniwa pamoja na mwalimu na mpenzi wa Kiswahili. Isitoshe, maswali yenye uzito na yanayohitaji upevu wa kimawazo yameshughulikiwa.

KUHUSU MWANDISHI

Mwalimu Onyango ni mwandishi wa msururu wa vitabu vya Dira; Dira ya Sarufi, Dira ya Ushairi na Dira ya Fasihi. Onyango Johnson pia ni Mwalimu wa Somo la Kiswahili katika shule ya Upili ya Wasichana ya Loreto. Aidha, ni mtafiti na mshirikishi wa Lugha ya Kiswahili katika Shirika la Habari la West, Kitengo cha Televisheni. Mwalimu pia ni mtahini wa karatasi ya tatu, 102/3; Fasihi.

TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa wapenzi wote wa lugha ya Kiswahili hasa masuala ya Fasihi. Walimu pamoja na watahiniwa wote wa mwaka huu wa 2020 pia sijawasahau. Mwalimu Joseph Otieno, Kakangu Dalmus Sakali, Mwalimu Josephat Wisyatsa na wengine wengi sina budi kuwashukuru kwa mchango wenu hasa katika uhakiki wa majbu ya kazi hii.

MAWASILIANO

Kwa Maoni, mapendekezo, malalamishi au utakapohitaji nakala ya majibu, tuwasiliane kwa njia ya simu 0707311302 au 0702771672 au katika barua pepe-johnsonoduory@gmail.com au katika kitandawazi-Mwalimu Onyango au instagramu-@mwalimu_onyango.

ILANI

Mtu yeyote hana ruhusa ya kuimiliki kazi hii bila ruhusa kutoka kwa, ni kinyume cha sheria za nchi na hata zile takatifu.

© 2020 MWALIMU ONYANGO 0707311302

SEHEMU YA KWANZA: RIWAYA YA CHOZI LA HERI

MASWALI 25 NA MAJIBU

1 "Maisha yangu yalijaa shubiri tangu utotoni."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (al. 4)
b) Kwa kutolea mfano, bainisha tamathali ya usemi inayojitokeza katika kauli hii. (al.2)
c) Jadili athari za vita katika jumuia ya Chozi la Heri (al.14)

2 Wanawake wamesawiriwa kwa mtazamo chanya katika jamii ya chozi la Heri. Jadili ukweli huu kwa kutoa ithibati mwafaka.
(al. 20)

3 "Ni mara ngapi mimi na babako husafiri na kukupagaza ulezi wa ndugu zako hawa? …umeweza kumuelekeza… katika kipindi hiki ambacho anatafuta utambuaji. Wewe pekee ndiwe dawa ya hasira … ya kivolkano. Bila wewe malezi ya hawa wadogo wako yangekuwa magumu."

a)Eleza muktadha wa dondoo hili. (al. 4)
b)Tambulisha mbinu tatu za sanaa zilizotumika katika dondoo hili. (al. 3)
c)Eleza sifa sita za mhusika "babako" aliyerejelewa katika dondoo hili. (al. 6)
d) "Ulezi ni ujima". Thibitisha kauli hii kwa kurejelea dondoo hili na riwaya yote kwa jumla.
(al. 7)

4 Jadili maudhui ya '**migogoro'** katika riwaya ya Chozi la Kheri. (al 20)

5 " …alinionya dhidi ya kumwambia yeyote kuhusu unyama…"

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al 4)
b) Fafanua sifa nne za anayehusishwa na maneno haya. (al 4)
c) Onyesha namna ukiukaji wa haki za watoto unavyotokea katika riwaya hii. (al 12)

6"…haifai kucheza na uwezo wa vijana, wao ni kama nanga. Huwezi kuzamisha na kuiongoa merikebu."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama4)
b) Bainisha tamathali mbili za usem izilizotumika katika dondoo. (alama 4)
c) Kwa kurejelea riwaya hii, onyesha jinsi vijana wamezamisha merikebu ya wahafidhina (alama12)

7 Baada ya dhiki faraja. Onyesha vile ukweli wa methali hii unavyodhihirika kwenye riwaya (alama20)

8. "Si kufua, si kupiga deki, si kupika…almuradi kila siku na adha"

a) a) Eleza muktadha wa kauli hii. (ala.4)
b) Taja mbinu mbili za kimtindo zilizotumika katika dondoo hili. (al.2)
c) Kwa kutumia hoja **kumi na nne**, eleza maudhui yaliyodokezwa na dondoo hili. (al.14)

© 2020 MWALIMU ONYANGO 0707311302

9 ”Kila mara hujiuliza ikiwa watoto huwa na hadhi tofauti nje au ndani ya ndoa” Amali inayotajwa imekumbwa na changamoto chungu nzima.Jadili kwa kurejelea riwaya nzima. (al.20)

10. “Kipi kilimpa mama uyabisi wa moyo hata akawaacha wanawe?”
(a)Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b)Bainisha tamathali moja ya usemi katika dondoo hili. (alama 1)
(c)Kwa kurejelea hoja kumi na tano kwenye riwaya, bainisha changamoto zinazoibuka kutokana na uyabisi wa wanawake. (alama 15)

11.“Alijihisi kama samaki aliyetiwa kwenye dema. Haya ni mazingira mageni kwake na hakuja hapa kwa hiari.”
(a)Onyesha jinsi wahusika wafuatao walivyotiwa kwenye dema kwa kurejelea riwaya ya Chozi la Heri.
(i) Pete (alama 6)
(ii) Dick (alama 6)
(iii) Subira (alama 4)
(iv) Selume (alama 4)

12. ‘Haya ni matokeo ya ubahimu wa binadamu’

a) Tia maneno haya kweny emuktadha wake (alama 4)
b) Eleza sifa sita za msemaji wa kauli hii (alama 6)
c) Kwa hoja kumi, Jadili ubahimu mwingine unaotendwa na binadamu riwayani (Alama 10)

13. ‘Baba umewahi kumwona <u>mtoto wa miaka hamsini ambaye hajasota</u>

;sikwambiikusimamadede?”

Jadili ukweli wa kauli iliyopigiwa mstari katika kauli ya hapo juu.Tumia hoja ishirini (Alama 20)

14 Alijiona kama mfa maji ambaye anakabiliwa na mtutumo wa mawimbi ya misiba, mmoja baada ya mwingine.

(a) Bainisha muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Eleza sifa tatu za anayerejelewa katika dondoo hili. (alama 3)
(c) Eleza tamathali ya usemi iliyotumika katika dondoo hili. (alama 2)
(d) Fafanua masaibu yaliyomkumba mrejelewa. (alama 3)
(e) Huku ukitolea mifano riwayani, jadili matatizo yanayowakumba wanajamii katika ndoa. (alama 8)

15 Eleza ufaafu wa anwani Chozi la Heri. (alama 20)

© 2020 MWALIMU ONYANGO 0707311302

16 “ Kwa kweli ni hali ngumu hii”

a) Weka dondoo katika muktadha wake. (alama4)
b) Ni hali gani ya msemewa inayorejelewa kwenye dondoo. (alama16)

17. “Lakini itakuaje historical injustice, nawe Ridhaa hapo ulipo sicho kitovu chako?

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Taja na utoe mifano ya mbinu za sanaa zilizotumika katika dondoo hili. (alama 4)
(c) Fafanua umuhimu wa msemaji wa maneno haya. (alama 2)
(d) Ni mambo gani yaliyowakumba wale ambao kitovu chao sicho walicho. (alama 10)

18. Uozo wa maadili ya jamii umekithiri katika Riwaya ya Chozi la heri, fafanua ukweli wa usemi huu. (alama 20)

19. "Mwanangu, usimpake tope baba yako. Amekulea kwa miaka yote hii kama mwanawe, japo kwa kweli hakuzaa wewe.”

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Kwa kurejelea wahusika wengine wanne wa kike katika riwaya, thibitisha matatizo manne yaliyowakumba katika jamii (alama 16)

20. Ukiukaji wa haki za binadamu ni jambo la kawaida katika chozi la heri. Jadili.(alama 20)

21. “Tangu lini mavi ya kale yakaacha kunuka?”

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
(b) Taja mbinu mbili za kimtindo zilizotumiwa katika dondoo hili (alama 2)
(c) Kwa kutumia hoja sita eleza mavi yanayozungumziwa katika dondoo hili. (al. 6)
(d) Kwa kutumia hoja nane eleza sifa nane za mrejelewa. (alama 8)

22..” …Mtu anayekusikiliza atadhani kwamba umekulia katika mazingira ambao uwepo wetu unaamriwa na matajiri.”

a)Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b)Fafanua sifa zozote nne za mrejelewa. (alama 4)

c)” Uwepo wa wanyonge uliamriwa na matajiri. Thibitisha ukirejelea hoja kumi na mbili katika riwaya ya Chozi la Heri. (alama 12)

© 2020 MWALIMU ONYANGO 0707311302

23.a)Maovu yametamalaki katika jamii ya riwaya ya Chozi la Heri. Thibitisha kauli hii ukirejelea mifano kumi kutoka kwa riwaya. (alama 10)

b)Fafanua nafasi ya vijana katika jamii ya Chozi la Heri. (alama 10)

24. "Nitapigana kwa jino na ukucha kuulinda utu wangu."

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Eleza umuhimu wa msemaji wa dondoo hili. (alama 4)

(c) Kwa kutolea mifano riwayani, thibitisha namna binadamu alivyopungukiwa na utu. (alama 12)

25. Mwanamke ametwezwa katika kiwango sawa na namna alivyotukuzwa. Thibitisha ukweli wa madai haya kwa kurejelea riwaya ya *Chozi la Heri.* (alama 20)

SEHEMU YA PILI: TAMTHILIA YA KIGOGO

MASWALI 20 NA MAJIBU

1. Majoka alitumia njia nyingi kudhibiti uongozi wake. Thibitisha ukweli huu. (alama 20)

2. **"**Tusiwaruhusu watu wachache waliojazwa kasumba….kuturejesha ….hatuwezi kukubali kutawaliwa kidhalimu tena."
   a. Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama4)
   b. Kwa kumrejelea mzungumzaji wa maneno haya, bainisha unafiki katika kauli hii. (alama 16)

3. Eleza jinsi mbinu ya taharuki ilivyotumika kufanikisha maudhui katika tamthilia ya kigogo. (alama 20)

4. "Sitaki kuaibishwa na mwanamke mimi, siwezi."

   a)Yaweke maneno haya katika muktadha wake. (alama 4)

   b)Fafanua kwa hoja nane kuwa msemaji wa maneno haya anafaa kuaibishwa (alama16)

5. a) Jadili jinsi kumi ambazo kwazo maudhui ya ukatili yanajitokeza katika tamthilia ya Kigogo (alama10)

© 2020 MWALIMU ONYANGO 0707311302

b) Eleza mifano mitatu ya matumizi ya kinaya katika tamthilia ya Kigogo (alama10)

6.”Acha porojo zako. Kigogo hachezewi; watafuta maangamizi!”

a)Eleza muktadha wa dondoo hili (al.4)

b)Fafanua sifa za mzungumzaji (al.6)

c)Kwa kurejelea hoja **kum**i, thibitisha kwamba kucheza na kigogo anayerejewa ni sawa na kutafuta maangamizi. (al.10)

7.”Tunahitaji kuandika historia yetu upya.”

a)Eleza sababu **kumi na mbili** kuonyesha kwa nini ilikuwa muhimu kuiandika historia ya sagamoyo upya (al.12)

b)Onyesha mikakati inayotumiwa kuiandika upya historia ya Jumuiya ya sagamoyo (al.8)

8“Na hiyo sauti ya Jabali imekuwa adha. Inanikama roho…..”

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili (Alama 4)

(b) Tambua mbinu mbili za lugh azilizotumika dondooni. (Alama 2)

(c) Kwa hoja kumi na nne, fafanua matendo mengine yanayomkama roho msemaji (Alama 14)

9 Eleza athari zozote kumi za tamaa na ubinafsi kwa kurejelea tamthilia ya kigogo. (Alama 20

10. Chombo chenye rubani imara huhimili vishindo na hasira ya mawimbi makali.

a. Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)

b. Tambua na ufafanue fani iliyotumika katika dondoo hili. (alama 2)

c. Onyesha jinsi msemewa alivyofeli kuhimili ‘vishindo na hasira ya mawimbi makali’ katika tamthilia hii. (alama 4)

d. Eleza kwa tafsili mambo yoyote **kumi** yanayokwaza usawa katika jamii ya *Kigogo*. (alama 10)

11 “Hivi vishahada vyao wanavyovipata siku hizi vinawavimbisha vichwa!”

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Taja tamathali zozote mbili zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)

© 2020 MWALIMU ONYANGO 0707311302

(c) Eleza changamoto zilizomkabili mrejelewa na wenzake. (alama 14)

12 Mwandishi wa Kigogo amefanikiwa sana katika matumizi yake ya mbinu ya jazanda na kinaya. Fafanua ukweli wa kauli hii kwa kurejelea tamthilia. (alama 20)

13”Waona mimi ni ganda la muwa la juzi”

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama4)

b) Tambuambinuyauandishiiliyotumikakatikadondoohili (alama2)

c) Thibitisha kuwa wahusika kadhaa wanalinganishwa na ganda la muwa katika tamthilia (alama14)

14 Anwani “KIGOGO”imetumika kitashtiti kumkejeli Majoka. Thibitisha (alama20)

15. “Asante ya punda kweli ni mateke. Sikujua ungekuja kunihangaisha……”

(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)

(b) Onyesha jinsi msemewa anamhangaisha msemaji. (alama 2)

(c) Kwa kurejelea tamthilia nzima, onyesha ukweli wa methali “Asante ya punda ni mateke. (alama 14)

16. Fafanua jinsi mwandishi wa tamthilia ya Kigogo alivyofaulu kutumia mbinu zifuatazo za uandishi. (alama 20)

(a) Jazanda
(b) Majazi

17)“Unayazika matumizi yetu .Unaifukia kesho yetu.”

a. Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b. Onyesha jinsi anayeambiwa maneno haya anavyoifukia kesho ya wenzake (alama 16)

18)Utawala wa majoka katika jimbo la sagamoyo umejaa sumu ya nyoka’’. Jadili ukweli wa usemi huu kwa kutoa hoja kumi (Alama 20)

© 2020 MWALIMU ONYANGO 0707311302

19. "Ukitaka kukula asali kaa na nyuki!"
    (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
    (b) Bainisha mbinu zilizotumika katika dondoo hili. (alama 4)
    (c) Eleza jinsi wahusika hawa walivyofaidi kutokana na kukaa na nyuki. (alama 2)
        (i) Chopi
        (ii) Kenga
        (iii) Ngurumu
        (iv) Mamapima

20. Eleza jinsi mwandishi wa Tamthilia hii ya Kigogo alivyotumia mbinu ya majazi. (alama 20)

SEHEMU YA TATU: DIWANI YA TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE

MASWALI 20 NA MAJIBU

1. "**Mapenzi Kifaurongo**"
    a) " Hadi sasa mimi ni kama rubani aliyeharibikiwa na ndege angani"
    Onyesha ukweli wa kauli hii ukirejelea hadithi nzima. (alama 10)

"**Shibe Inatumaliza**"

    b) "Hatuwezi kumaliza kula. Kila leo tunakula . Hiki na kile…"
    Fafanua dhana ya ulaji kama inavyojitokeza kwenye hadithi hii. (alama 10)

2. " **Ndoto ya Mashaka**"
    Mwandishi wa hadithi hii anatupa taswira ya jamii iliyozongwa na masaibu yanayotamausha. Tetea ukweli wa kauli hii. (alama 20)

3. *Masharti ya kisasa* ni anwani mwafaka ya hadithi hii. Fafanua.
    (Alama 20)

4. " Kwa nini wasiwe na uhuru wa kuvaa wanavyopenda? Au huelewi wanawake wana uhuru? "
    a) Weka maneno haya katika muktadha wake. (Alama 4)
    b) Eleza sifa tatu za msemewa (Alama 6)
    c) Thibitisha ukweli kuwa wanawake wana uhuru kwa mujibu wa hadithi.

© 2020 MWALIMU ONYANGO 0707311302

5. Eleza nafasi ya vijana katika jamii ukerejelea hadithi fupi zifuatazo.

a) Mapenzi ya kifaurongo (alama 5)

b) Shogake Dada ana Devu (alama 5)

c) MameBakari (alama10)

6. Ndoto yamashaka: Ali Abdalla Ali

"Sasa nimechoka mja.Nimechoka hata na radua kufa kuliko kuishi.Hadi lini haya mashaka ya kutengenezwa?Mashaka ya mashaka!

a) Elezamuktadhawadondoohili (alama 4)

b) Tambuambinumbilizalughazilizotumika (alama 4)

c) Fafanua mambositayanayomfanyamrejelewaaraduekufa. (alama12)

7. "Madhila ya mtoto mvulana katika karne ya ishirini na moja ni mengi." Tetea kauli hii kwa hoja ishirini ukirejelea hadithi ya *Mapenzi ya Kifaurongo*, *Masharti ya Kisasa* na *Ndoto ya Mashaka*. (alama 20)

8. **Salma Omar:** ***Shibe Inatumaliza***

(a) " Sijali lawama mnonilaumu"

(i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(ii) DJ na wenzake wanaonekana kufurahia maudhui ya wimbo huu. Thibitisha. (alama 6)

(b) **Alifa Chokocho:** ***Shogake Dada ana Ndevu***

"…tumshukuru kwa jinsi alivyomwongoza na kumwelekeza kwenye njia iliyonyooka" Ukirejelea wasifu wa Safia, tetea na upinge kauli hii. (alama 10)

9. "Unafikiria mambo mabaya… unafikiria mambo maovu!"

a) Weka dondoo hili katika muktadha ukirejelea 'shogake Dada ana Ndevu' alama 4

b) Ni mambo yapi aliyofikiriwa mzungumzaji? Alama 2

c) Eleza sifa za mzungumzaji na ufafanue umuhimu wake alama 14

© 2020 MWALIMU ONYANGO 0707311302

10. Nizikeni papa hapa – Ken Walibora

"Ndugu yangu tahadhari na hawa....."

a) Eleza muktadha wa dondoo (al.4)

b) Eleza sifa za msemewa (al.4)

c) Taja na ufafanue maudhui sita katika hadithi hii (al.12)

11. a) Tulipokutana Tena – Alfa Chokocho

Jadili jinsi maudhui ya umaskini yalivyoshughulikiwa katika hadithi ya 'Tulipokutana Tena'.

(al. 10)

Mame Bakari

b) Kina dada wanaobakwa wanakabiliwa na change moto nyingi. Tetea. (al. 10)

12."Penzi lenu na nani? ……. Mgomba changaraweni haupandwi ukamea. Potelea mbali wee!"

a)Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b)Taja na ufafanue mbinu za lugha zilizotumiwa katika dondoo hili. (alama 4)

c)Onyesha vile maudhui ya utabaka yanavyojitokeza katika hadithi nzima. (alama 6)

d)Eleza sifa za mzungumzaji. (alama 6)

13.Sekta ya elimu imekubwa na changamoto nyingi. Thibitisha ukirejelea hadithi zifuatazo:

a)Mapenzi ya kifaurongo.

b)Shogake dada ana ndevu.

c)Mwalimu mstaafu.

d)Mtihani wa maisha. (alama 20)

© 2020 MWALIMU ONYANGO 0707311302

Kwa kuzingatia hadithi zifuatazo nne katika diwani ya Tumbo lisiloshiba na Hadithi nyingine, thibitisha ukweli wa kauli hii.

(i) Tumbo lisiloshiba
(ii) Mapenzi ya kifaurongo
(iii) Ndoto ya mashaka
(iv) mkubwa

15) "Hatuwezi kumaliza kula,kila leo tuna kula"

(a)Eleza mukadha wa dondoo hili. (alama4)

(b)Fafanua tamathali ya usemi iliyotumika. (alama 2)

(c)Eleza umuhimu wa mnenaji. (alama 4)
(d)"Lakini na kwambia tena,kula kunatumaliza"Kwa kudokeza hoja kumi ,jadili ukweli wa Kaul hii. (alama 10)

16. Kwa kurejelea hadithi zozote tano katika diwani ya, 'Tumbo lisiloshiba na hadithi nyingine.' Jadili maudhui ya nafasi ya wazazi katika malezi. (alama 20)

17."…hamna mwendawazimu wala mahoka kati yetu, mimi nimepewa zawadi hizo"

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (al.4)
b) Eleza sifa nne za msemaji (al.4)
c) Hakiki nafasi ya maudhui ya busara kwa mujibu wa hadithi hii (al.12)

18. "Kwetu tunapigania mikono ielekee vinywani. Mzoea vya sahani, vya kigae haviwezi."
(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Bainisha tamathali moja ya usemi kwenye dondoo hili. (alama 12)
(c) Jadili maudhui ya utabaka ukirejelea hadithi hii. (alama 14)

19."Ubadhirifu wa mali ya umma umetamalaki katika hadithi ya shibe inatumaliza. Jadili. (alama 20)

20)Kwa kuzingatia hadithi zozote tano ,eleza uozo wa jamii kama unavyojitokeza katika tumbo lisiloshiba na hadithi nyingine.

SEHEMU YA TATU: FASIHI SIMULIZI

© 2020 MWALIMU ONYANGO 0707311302

MASWALI 15 NA MAJIBU

1.

a) Huku ukitoa hoja sita linganisha aina mbili kuu za fasihi. (alama6)
b) Jadili vipengele sita vya kuzingatia katika uchanganuzi wa hadithi.(alama6)
c) Jadili sifa mbili za vitanza ndimi kwa kurejelea sauti. (alama 2)
d) Tambua dhana zinazotokana na maelezo haya.

i. Msimulizi wa fasihi simulizi anaitwaje kwa jumla? (alama1)
ii. Shujaa katika mighani pia anaweza kuitwa nani? (alama 1)
iii. Sherehe za kitamaduni ambazo hufungwa na jamii katika kipindi fulani maalum huitwaje? (alama 1)
iv. Mavazi au vifaa vinavyotumiwa na wasanii kuakisi hali halisi ya mambo wakati wa kuwasilisha fasihi huitwa(alama 1)
v. Mtambaji wa hadithi hutumia ujuzi gani anapoibadilisha hadithi yake moja kwa moja mbele ya hadhira bila kuathiri usimulizi wake?(alama 1)
vi. Wanaosimuliwa ili kuonyesha kazi ya fasihi simulizi hupewa jina hili.(alama 1)

2

a) i) Semi nini? (alama 1)

ii) Fafanuasifannezamisimu (alama4)

b) Soma wimboufuataokishaujibumaswali

Ewe kilizi

Ulozoweakujificha

Nyumaya mama kujikinga, dhidiyamilio

Yanadiilojuumbinguni

Juakeshonisikuyasiku

Sikuyakujuambivunambichi

Kutofautishajogoonavipora

Naribatakaposhika, chakekisu

Ndipoutakapojuabayana

Ukoowetusiwakunguru

ikiwahutayari

kisukukidhihaki

sithubutukamwe, wanjanikuingia

© 2020 MWALIMU ONYANGO 0707311302

sijekuniaibishamiye, amiyonaakrabanzima!

Maswali

i) Huuwimbohuitwaje? (alama1)

ii) Elezamajukumuyoyotemanneyanayotekelezwanawimbohuukatikajamii(alama4)

c) i) Mivighaninini? (alama2)

ii) Elezasifatatuzamivigha (alama 3)

d) Fafanuamatatizomatanoambayoyanaikumbwafasihisimuliziduniani (alama5)

3

a) ”Mwanangu nakuomba uzingatie uadilifu maishani uongofu ni nuru ya mustakabali wa kila mtu…”

i)Tambua kipera na utanzu wa tungo hili (al. 2)

ii)Kwa kutumia hoja **mbili** eleza muundo wa kipera hiki (al. 2)

iii)Fafanua sifa **nane** za kipera hiki (al.8)

b) Eleza vikwazo **vinane** vya ukuaji wa fasihi simulizi. (al.8)

4. 1)

i)Ni nini maana ya ulumbi katika fasihi simulizi [alama 2]

ii)Fafanua umuhimu wa ulumbi (alama4)

iii)Eleza sifa nne za ulumbi(alama4)

2) Tofautisha baina ya

i)Hurafa na Hekaya (Alm4)

ii)Hadithi za mazimwi na Hadithi za mtanziko (alm 4)

iii)usuli na visaasili (alama2)

5. “Magwiji wa uwanda mpana wa tamaduni za Kiafrika: wazee walioila chumvi wakabobea katika falsafa za turathi zetu, maghuluma wenye misuli tinginya na vifua vya mfumbata vinavyostahimili hujuma za kila nui na malaika wa kike ulioshehenimizinga na chemichemi ya urembo, nawasabahi. Wa zamani waliamba kuwa mwacha mila ni mtuma. Turathi zetu ni uhai. Turathi zetu ni msingi wa ubinadamu wetu. Turathi zetu zinabeba mustakabali wetu. Tuzienzi kama tuenzivyo asali.”

Maswali

© 2020 MWALIMU ONYANGO 0707311302

(a) (i) Tambua kipera cha utanzu wa mazungumzo kinachohusishwa na kifungu hiki. (alama 1)

(ii) Thibitisha jibu lako katika (i) kwa mifano yoyote **mitatu**. (alama 3)

(b) Iwapo umehudhuria utendaji wa kipera hiki nyanjani eleza sifa **tano** za mtendaji utakazoziona zisizojitokeza kwenye kifungu. (alama 5)

(c) Taja na kueleza miktadha **minne** ambamo kipera hiki kinaweza kutumiwa katika jamii ya kisasa. (alama 4)

(d) Andika sifa zozote **nne** za jamii ya nafsi neni katika utungo huu. (alama 4)

(e) Eleza njia **tatu** za ukusanyaji wa data unazoweza kutumia kukusanya data kuhusu kipera hiki. (alama 3)

6 Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Mtu A: Tulienda kwa hiyo sherehe jana…

Mtu B: Ooh! Kumbe ulipata ngiri mbili za kiingilio?

Mtu A: Nilivaa chupa woiyee!

Mtu B: Ulimuona yule kijana Kamba?

Mtu A: Hehehe! Yule huringa mbaya…

Mtu B: Huyo alitoka mbio aliposikia kumethuka…

Maswali

(a) Tambua kipera cha utanzu wa semi kinachohusishwa na kifungu hiki. (alama 1)

(b) Fafanua umuhimu wa kipera hiki. (alama 5)

(c) Ngomezi ni nini? (alama 2)

(d) Jadili sababu ambazo zimesababisha kuzorota kwa matumizi ya ngomezi katika jamii ya kisasa. (alama 6)

(e) Jadili sifa za sogora zinazojitokeza nyanjani wakati wa utafiti. (alama 6)

7. (a) (i) Ni nini maana ya ngomezi (alama 2)

© 2020 MWALIMU ONYANGO 0707311302

(ii) Fafanua sifa tano za ngomezi (alama 5)

(iii) Taja mifano mitatu ya ngomezi kisasa (alama 3)

(b) (i) Bainisha aina nne za watendaji wa fasihi simulizi (alama 4)

(ii) Eleza sifa sita bainifu za mtendaji fasihi sismulizi (alama6)

8. (a) Eleza sifa nne za kimtindo zinazopatikana katika methali za Kiswahili. (alama 8)

(b) Eleza mbinu tatu ambazo hutumiwa kuzua misimu. (alama 6)

(c) Ni jukumu la jamii kudumisha fasihi simulizi. Dhihirisha. (alama 6)

9. Jadili jinsi mwigizaji anaweza kuboresha utanzu wake jukwaani. (alama 20)

10. a) Taja aina nne za malumbano ya utani. (alama 4)

b) Eleza sifa nne za malumbano ya utani. (alama 8)

c) Fafanua dhima ya malumbano ya utani. (alama 8)

iii) Eleza sifa nne za maigizo. (alama 8)

iv) Ni upi umuhimu wa maigizo? (alama 6)

11. a) Fafanua maana ya lakabu. (Alama 3)

b) Sifa za lakabu ni zipi? (Alama 5)

c) Kwa nini lakabu ni muhimu katika jamii? (Alama 2)

d) Jadili manufaa ya utafiti katika fasihi simulizi. (Alama 10)

12. a) Eleza kipera cha mawaidha. (Alama 2)

b) Fafanua sifa tano za mawaidha. (Alama 10)

c) Mawaidha yana umuhimu gani katika jamii. (Alama 8)

13)a)Fafanua sifa tatu za kila mojawapo ya vipera vya fasihi simulizi vifuatavyo (alama 6)

(i) Vitendawili

(ii) Methali

b.Mawaidha yana dhima gani katika jamii? Eleza (alama 6)

© 2020 MWALIMU ONYANGO 0707311302

c.Bainisha sifa za nyimbo. (alama 4)

d.Eleza umuhimu wa nyimbo za kisiasa (alama 4)

14. (a) Taja sifa tanzu zifuatazo za fasihi simulizi.
    (i) Hurafa (Alama 2)
    (ii) Mighani
    (Alama)
    (iii) Miviga (Alama 2)
    (b) Eleza umuhimu wa ngomezi katika jamu. (Alama 6)
    (c) Eleza sifa nne za mafumbo. (Alama 4)
    (d) Eleza tofauti mbili kati ya malumbano ya utani na mawaidha. (Alama 4)

15. Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali uliyoulizwa.

Hapo zamani za kale mamba na tumbiriwalikuwa marafiki wakubwa sana. Siku moja mamba akamwendea rafiki yake tumbiri na kumwambia “Rafiki yangu” Tumbiri akaitikia “Naam” Mamba akajiandaa na kusema, “Siku zote mimi ndiye nijaye nchi kavu kukutembelea Mbona wewe huji kwangu majini kunitembelea?” Tumbiri akawaza na kujibu, “sasa nitakuja vipi mimi na sijui kuogelea?’Mamba akaniwambia, “Ahh hilo tu? Panda mgongoni kwangu, nitakuchukua mpaka nyumbani.” Tumbiri akapanda, safari ya kwenda kwa mamba ikaanza.

Wakaenda pa! pa! pa! walipofika katikati ya mto mamba akamwambia, “Si unajua rafiki kuwa ninakupenda sana?” Tumbiri akaitikia, “Naam!” Mamba akaendelea, “Sasa huko kwetu mtu akimpenda mwingine sana hula moyo wake. Basi nipe moyo wako niule!” Tumbiri akawaza, akawaza wee mpaka akapata la kusema. “Ahh moyo wangu? Mbona basi hukuniambia tangu hapo? Mimi kawaida huuacha moyo wangu nyumbani. Basi turudi nikakuchukulie rafiki yangu”. Mamba akageuka paap! Akarudi nchi kavu huku ana matumaini makubwa. Tumbiri akachapa mbio na kukimbilia mtini. Alipokuwa huko juu akatunda embe na kumrushia mamba akisema, “Moyo wangu huo!” Mamba akalikimbilia embe hilo kwa kudhani ni moyo wa tumbiri. Alishindwa kuuona moyo huo kutokana na matope ya mtoni. Mpaka leo mamba anaonekana akizunguka kuutafuta moyo wa tumbiri. Tumbiri naye hathubutu tena kumkaribia Mamba.

© 2020 MWALIMU ONYANGO 0707311302

MASWALl

a) i) Hii ni ngano ya ama gani? (alama 1)

ii) Je, ni wasifu gani wa kitabia unawakilishwa na mamba? (alama 3)

iii) Eleza sifa **tatu** kuu zinazohusishwa na ngano a fasihi simulizi katika ngano hii (alama 3)

iv) Ikiwa utaiwasilisha ngano hii mbele ya hadhira ni mambo gani utakayosisitiza katikauwasilishaji huo? (alama 3)

b) (i) Eleza umuhimu wa vitanza-ndimi (alama 2)

(ii) Taja sifa **mbili** za vitendawili (alama 2)

(iii) Taja na uelezee umuhirnu wa vitendawili (alama 6)

© 2020 MWALIMU ONYANGO 0707311302